

## **CHUO CHA UONGOZI WA MAHAKAMA CHATOA MAFUNZO KWA MAOFISA WA NSSF.**

Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA) kimeendesha mafunzo kwa maofisa mbali mbali 30 wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF).

Mafunzo hayo ya siku kumi (10) yalifanyika katika ukumbi wa Bandari mjini Tanga na yalikuwa na lengo la kuwajengea uwezo na weledi maafisa ambao wote ni wanasheria lakini wametoka vitengo mbali mbali namna bora ya kuendesha mashtaka chini ya sheria inayoanzisha mfuko huo yaani NSSF Act.

Mafunzo hayo yalitolewa na wawezeshaji kutoka Mahakama ya Tanzania, Mamlaka ya Usimamizi wa Mifuko ya Jamii (SRRA), Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka(DPP), Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto na Jeshi la Polisi. Baadhi ya maeneo yaliyofundishwa ni pamoja na uendeshaji wa mashtaka katika makosa ya mitandao (Cyber crime), marekebisho ya sheria za mifuko ya jamii, marekebisho yanayohusu Ofisi ya Mwanasheria wa Serikali, upelelezi na uendeshaji wa mashtaka kwa ujumla.

Mafunzo hayo yaliandaliwa na Chuo kama sehemu ya kutimiza wajibu wake wa kuwajengea uwezo wadau wa sekta ya sheria katika kutimiza majukumu yake. Mafunzo hayo yalifunguliwa na Mkuu wa Chuo Mhe Jaji Dkt Paul Kihwelo na kufungwa na Jaji Mfawidhi Mahakama ya Tanga Mhe Jaji Iman D Aboud.